

## SWALA YA MLINZI WAKATI AKIWA KAZINI

### (1) SWALA YA JAMAA NA IJUMAA KWA MLINZI:

Aliulizwa Sheikh Ibnu Baaz Allah amrehemu kuhusu uwajibu wa kuswali jamaa kwa mlinzi ambaye yupo katika kazi ya kulinda nyumba au ofisi na kadhalika, je aache kulinda aelekee msikitini kuswali jamaa ya swala za Faradhi za kutwa na za Ijuma au nini afanye?

لا، الحراسة عذر، الحارس على الشيء المهم الذي يخشى عليه، ليس له أن يدعه ويذهب إلى صلاة الجمعة والجماعة، بل عليه أن يصلي في محله، ويسقط عنه حضور الجمعة والجماعة في هذه الحال، إلا إذا وجد من ينوب عنه ممن لا جمعة عليه: كالمملوك والنساء وأشباه ذلك، نعم.

### Akajibu:

“ Hapana, Ulinzi ni udhuru (wa kutohudhuria jamaa msikitini) , mlinzi wa kitu chenye umuhimu (chenye thamani) kinachoogopewa (kupotea au kuibiwa) haifai kwake kukiacha na kuelekea msikitini kwa ajili ya swala ya jamaa na ya Ijuma, bali anatakiwa aswali katika eneo alipo, na unaporomoka uwajibu wa kuhudhuria swala za Ijuma na Jamaa katika hali kama hii. Isipokuwa (atawajibika kwenda kuswali katika jamaa) endapo atapata mtu wa kumuachia miongoni mwa wale ambao hawana uwajibu wa kuswali Ijuma kama vile Watumwa na Wanawake na mfano wa hao, ndio. “

### (2) HUKUMU YA MLINZI KUSWALI NJE YA WAKATI

Aliulizwa Sheikh Ibnu Baaz Allah Amrehemu: Je anapata dhambi mlinzi ambaye ameacha kuswali swala ya Alasiri mpaka muda wake ukapita akasali baada ya kuingia magharibi kwa sababu ya kukosa mtu wa kumuachia ulinzi ili aende kuswali msikitini ?

لا يجوز للحارس وغيره أن يؤخر الصلاة عن وقتها؛ لقوله تعالى: إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا [النساء: 103] أي: مفروضة في الأوقات، ولأدلة أخرى من الكتاب والسنة وعليه أن يصلي الصلاة في وقتها مع قيامه بالحراسة، كما صلى المسلمون مع النبي ﷺ صلاة الخوف وهم مصافون للعدو، والله ولي التوفيق.

### Akajibu:

“ Haifai kwa mlinzi na asiyekuwa mlinzi kuchelewesha swala mpaka ukapita muda wake; kwa kauli yake Allah Mtukufu: ((Hakika swala kwa waumini ni jambo lenye wakati maalumu)) Annisaa 103; yaani zimefaradhiwa katika nyakati maalumu. Sambamba na dalili nyingine zilizomo ndani ya Qur'an na Sunna. Ni wajibu juu ya mlinzi aswali ndani ya muda wake pamoja na kusimamia ulinzi wake, kama ambavyo maswahaba walivyoswali pamoja na Mtume swallallahu alaihi wasallam swala ya wakati wa hofu wakiwa wamepanga safu kuelekea maadui vitani, na Allah ndiye msimamizi wa Taufiq. “

المرجع: مجموع فتاوى ابن باز والموقع الرسمي له